Al-imad Journal of Humanities and Applied Sciences (AJHAS)
مجلة العماد للعلوم الإنسانية والتطبيقية
ISSN: 3106-0323
Volume 2 – Issue 1 – 2026
Pages 1152-1158

# DHAMIRA YA BINADAMU KUTENDA WEMA KATIKA DIWANI YA MASHAIRI YA SAADANI

Hamad Jabir Bashir * [1], Mohamed Omary Maguo [2]
[1,2] Department of Linguistics and Literary Studies, the Faculty of Arts and Social Sciences, The Open University Dar es Salaam, Tanzania
*Corresponding: hamadjabr90@gmail.com

## تمثلاتُ فعلِ الخير الإنساني في ديوان «*Mashairi ya Saadani*» للشاعر سعدان عبدو كندورو

حمد جبر يشير [1]*، محمد عوماري ماقو [2]
[1،2] قسم اللغويات والدراسات الأدبية، كلية الآداب والعلوم الاجتماعية، الجامعة المفتوحة دار السلام، تنزانيا

Received: 29-04-2026; Accepted: 02-06-2026; Published: 16-06-2026

**Ikisiri**
Makala haya yanahusu kuchunguza dhamira ya binadamu kutenda wema katika diwani ya Mashairi ya Saadani iliyoandikwa na Saadan Abdu Kandoro mwaka 1972. Data za makala haya zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini ambapo walisoma kwa makini diwani ya Mashairi ya Saadani kwa kuzingatia lengo la makala na kuweza kupata data za utafiti. Baada ya kukusanya data hizo za utafiti zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo. Makala yanaonesha kwamba katika diwani ya Mashairi ya Saadani kunawasilishwa dhamira ya kutenda wema ambapo binadamu anasisitizwa kutenda wema hata kwa watu ambao wamemfanyia ubaya kupitia mashairi mawili. Hakika huu ni msisitizo adhimu wa kuonesha umuhimu wa dhamira hii katika jamii.

**Mneno Mkuu:** Maana za kimaadili, uwakilishi wa wema, diskosi ya kishairi ya Kiswahili, maadili ya kibinadamu, Diwani ya Mashairi ya Saadani ya Saadani Abdu Kandoro**.**

**الملخص**
تتناول هذه المقالة استقصاء قيمة الاحسان على فعل الخير في ديوان «*Mashairi ya Saadani*»للشاعر السواحلي سعدان عبدو كندورو، الصادر عام 1972م. وقد جُمعت بيانات الدراسة بالاعتماد على منهج القراءة التحليلية المتعمقة؛ إذ قمنا بقراءة الديوان قراءة دقيقة وممنهجة في ضوء أهداف الدراسة، بغية استخراج المعطيات المرتبطة بموضوع البحث، وبعد جمع البيانات، جرى تحليلها باستخدام المنهج الوصفي التحليلي. وتكشف نتائج الدراسة أن الديوان يقدّم رؤية أخلاقية وإنسانية تؤكد قيمة الإحسان وفعل الخير، حيث يدعو الإنسان إلى التحلّي بالفضائل ومقابلة الإساءة بالإحسان حتى تجاه من ألحقوا به الأذى، وهو ما يتجلى بوضوح في قصيدتين من قصائد الديوان. وتبرز هذه المعالجة الشعرية الأهمية البالغة لهذا المبدأ الأخلاقي في بناء مجتمع متماسك تسوده قيم التسامح والتراحم والتعايش الإنساني.

**الكلمات المفتاحية**: الدلالات الأخلاقية، تمثلات الخير، الخطاب الشعري السواحيلي، القيم الإنسانية، ديوان سعدان عبدو كندورو.

## 1.1 Utangulizi

Ushairi ni utanzu mkongwe katika fasihi. Utanzu huu una historia ndefu sana tokea enzi na enzi, katika fasihi ya Kiswahili (Wamitila 2008). Ingawa mpaka leo hii hakuna makubaliano kuhusu utungo wa mwanzo wa kishairi uliandikwa lini, lakini wataalamu wanakubaliana kuwa

 Copyright: © 2026 by the authors. Submitted for possible open access publication under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution (CC BY) license (https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/).

historia yake ni ndefu. Wengi wanakubaliana kuwa utungo wa mwanzo ni Utendi wa Mwana Munga, unaodaiwa kuandikwa na Fumo Liyongo 1517 (Mulokozi na Sengo (1995).

Shairi ni utungo wa sanaa uliowasilishwa kwa maneno wenye mpangilio maalumu wa mishororo na kisauti uliowasilishwa kwa maneeno mateule kwa kutumia nbinu za lugha ya mnato na mbinu nyengine za kibalagha na kimtindo zinazomwezesha mtunzi kuwasilisha ujumbe kwa ufupi, na unaoeleza kisa, hisia, tukio au hali kwa lugha ya mvuto (Njogu na Chimerah, 1999).

Ushairi wa Kiswahili una makundi mawili makuu, mashairi ya jadi au mapokeo ambayo yanatungwa kwa kuzingatia arudhi au kaida za utunzi wa (mashairi) kama vina, mizani, idadi maalumu ya mishororo na vipande katika ubeti. Kundi la pili ni mashairi ya kisasa ambayo hayafuati kanuni yoyote (Wamitila, 2008). Ushairi wa Kiswahili ulianza kwa njia ya nyimbo, na ndiyo yaliyokuwa mashairi ya kwanza.

Lugha ina nafasi kubwa katika ushairi. Ushairi unajitafautisha zaidi na tanzu nyingine kwa namna ambavyo unatumia lugha. Sifa hii ya matumizi ya lugha hutokana na kaida ya ushairi wenyewe. Kaida zinazotumika na ushairi ni kama vina, mizani, mpangilio wa kibalagha, beti, mishororo, takriri sauti nk.

Wahakiki wengi hutofautisha utanzu huu wa ushairi kutokana na kigezo cha muundo na matumizi ya lugha. Sifa kuu zinazotumiwa ni matumizi ya lugha ya kishairi, vina na mizani nk. Ushairi hutumia msamiati teule, tamathali za kibalagha na dhamira. Uteuzi wa maneno au msamiati ni muhimu katika ushairi. Mshairi hana fursa za kueleza dhamira zake au maudhui kama anavyoeleza katika kazi ya kinathari. Katika ushairi maneno yana uzito maalumu.

Mashairi yanasifa yakutumia ishara, jazanda au maelezo yake kuwa na maana nyingi, na kuashiria jambo jengine. Jazanda ni matumizi ya taswira, huwa na maneno ya kuashiria jambo fulani (Wamitila, 2008). Mbinu hizi humpelekeya mshairi kufikisha ujumbe bila kutumia maneno mengi. Yakitokea hayo, nilazima muhakiki ajiulize maneno yaliotumika yana maana gani. Uchunguzi wa taswira na jazanda lazima uchunguze picha za kiakili.

Kama ilivyoelezwa hapo mwanzo kuwa ushairi una historia ndefu, na kustawi kifani. Hapo awali ushairi wa Kiswahili ulikuwa ukitungwa kimasimulizi na baadaye ukaanza kutungwa kimaandishi miongoni mwa jamii ya Waswahili zilizoishi katika upwa wa Afrika Mashariki. Ushairi wa Kiswahili ulitungwa kwa kuzingatia utamaduni na jamii pana (Senkoro, 1988). Kwa njia ya ubunifu, ushairi wa Kiswahili unakuwa ni nguzo ya kusawiri na kuwasilisha uhalisia wa maisha ya wanajamii katika miktadha mahsusi ya kitamaduni.

Kadhalika, ushairi wa Kiswahili ulikuwa katika masimulizi na kuwasilishwa kama nyimbo au kughaniwa, baadaye ukaanza kutungwa na kuhifadhiwa kimaandishi (Babusa, 2005). Pia, ushairi unapokaririwa au kusomwa kwa sauti unabainisha matumizi ya lugha ambayo ni ya kiwango cha juu cha usanii, hasa unapolinganishwa na tanzu nyengine kama vile riwaya, hadithi fupi na tamthiliya. Mshairi wa Kiswahili ana uhuru mkubwa katika matumizi ya msamiati, uumbaji wa miundo mbali mbali na tamathali za lugha. (Senkoro, 1988) anakariri kwamba, kinachofanya maudhui kuwa muhimu katika ushairi wa Kiswahili ni uwasilishwaji wake kupitia ishara maalumu za lugha zinazojengeka katika tamathali za usemi. Kutokana na matumizi mahsusi ya lugha na mbinu za uwasilishaji, ushairi wa Kiswahili huiathiri na kuigusa mioyo ya hadhira (Mulokozi na Sengo, 1995).

Ushairi wa Kiswahili ni utanzu ambao umechunguzwa na watafiti wa ndani na wa nje ya bara la Afrika. Mfano, watu waliowahi kushughulikia mada ya ushairi ni hawa wafuatao. Abeid (1954), Kezilahabi (1974; 1977), Kahigi na Mulokozi (1979), Senkoro (1988), Mulokozi (1975), Njogu na Chimerah (1999), Kitogo (2002), Masinde (2003), Babusa (2005) na Omary (2011; 2015). Kutokana na tafiti za wataalamu hawa, waandishi wa makala haya wamevutiwa kuchunguza dhamira ya kutenda wema katika diwani ya *Mashairi ya Saadani* ambayo iliandikwa katika kipindi cha utekelezaji wa Azimio la Arusha na siasa za ujamaa na kujitegemea.

 Copyright: © 2026 by the authors. Submitted for possible open access publication under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution (CC BY) license (https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/).

## 1.2 Tatizo la Makala

Licha ya kuwapo kwa tafiti nyingi zilizochunguza ushairi wa Kiswahili kwa kuzingatia vipengele vya fani na maudhui, bado kuna upungufu wa tafiti zilizojikita mahsusi katika kuchunguza namna dhamira ya kutenda wema inavyosawiriwa katika diwani ya *Mashairi ya Saadani* ya Saadan Abdu Kandoro. Tafiti nyingi zilizotangulia zimejikita katika masuala ya kisiasa, kijamii na kifalsafa katika ushairi wa Kiswahili, huku dhamira ya kutenda wema na mchango wake katika kujenga maadili ya jamii ikipewa nafasi ndogo. Kutokana na pengo hilo la kiutafiti, **makala haya yanakusudia kuchunguza namna dhamira ya kutenda wema ilivyowasilishwa katika diwani ya *Mashairi ya Saadani* na umuhimu wake katika jamii.**

## 1.3 Umuhimu wa Makala

Makala haya yana umuhimu wa kitaaluma na kijamii. Kitaaluma, yatachangia kuongeza maarifa kuhusu uchambuzi wa dhamira za maadili katika ushairi wa Kiswahili, hususan katika kazi za Saadan Abdu Kandoro. Aidha, yataongeza marejeleo kwa watafiti na wanafunzi wanaojihusisha na fasihi ya Kiswahili. Kijamii, matokeo ya makala haya yatasaidia kuonesha nafasi ya ushairi katika kuhimiza maadili mema, mshikamano wa kijamii, upendo na huruma miongoni mwa wanajamii.

## 1.4 Maswali ya Makala

1. Dhamira ya kutenda wema imewasilishwaje katika diwani ya *Mashairi ya Saadani* ya Saadan Abdu Kandoro?
2. Dhamira ya kutenda wema iliyojitokeza katika diwani ya *Mashairi ya Saadani* ina umuhimu gani katika kujenga maadili na mahusiano mema katika jamii?

## 2.1 Kiunzi cha Nadharia

Makala haya yameongozwa na nadharia ya Sosholojia ya fasihi ambayo ni muafaka katika kuchambua mambo ya kifasihi. Nadharia ni muongozo ambao ndiyo unatoa picha kamili ya namna na aina ya data za utafiti zitakazokusanywa na kuchambuliwa.

### 2.1.1 Nadharia ya Sosholojia ya fasihi

Nadharia ya Sosholojia ni moja kati ya nadharia ambazo zinatumika katika kuchambua masuala ya kijamii katika taaluma mbalilmbali zikiwemo taaluma za fasihi. Nadharia hii imeasisiwa na mwanasosholojia Auguste Comte, ambaye alikuwa akichunguza mivutano ya kijamii ambayo imeletwa na maendeleo ya uchumi wa viwanda na mambo ya kijamii kwa ujumla wake (Wamitila, 2002). Sosholojia ni nadharia ambayo inaeleza kuwa jamii huishi katika mahusiano ya kitabaka ambapo kuna matabaka katika kila sekta. Katika sekta ya viwanda kuna waajiri ambao ni wanaweza kuwa ni wamiliki, mabosi, waajiriwa, vibarua na walinzi. Ikiwa ni katika masuala ya kijamii kuna viongozi, matajiri, watu masikini, kuna wakulima, wafanyakazi, wafanyabiashara, viongozi wa dini, waumini na wasiokuwa waumini. Watu katika makundi haya hushirikiana na kutegemeana katika shughuli zao za kila siku. Katika mashirikiano na mahusiano hayo huibuka mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na migogoro, maelewano, ndoa, watukutu na wakorofi, walevi, wezi, majambazi, na kila aina ya mema na mabaya pia.

Nadharia ya Sosholojia inayaona matokeo haya ya mahusiano yaliyopo katika jamii kuwa ndio mambo ambayo yanasukuma jamii na kuendelea au kuwa katika hali iliyopo. Maisha ya jamii yanakuwa siku hata siku kwa sababu ya mahusiano haya ya kijamii katika sekta mbalimbali pamoja na matokeo ya mahusiano hayo. Kimsingi, ili maisha yaendelee na yawepo ni lazima mambo haya yote yaweze kufanyika ingawa kuna mengine kama ya wizi na ujambazi hayatakiwi kuwepo kwa kiasi kikubwa kwa sababu yana hatarisha usalama wa maisha ya watu.

 Copyright: © 2026 by the authors. Submitted for possible open access publication under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution (CC BY) license (https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/).

Nadharia ya Sosholojia tawi la fasihi kwa ujumla wake nalo pia linaangalia uhusiano uliopo baina ya fasihi ya jamii ambapo inabainika kuwa uhusiano wa fasihi na jamii ni wa wazi sana (Njogu na Chimerah, 1999). Fasihi ni zao la jamii ikiwa na maana kuwa haitatokea kuwa na fasihi bila kuwa na jamii. Ni katika jamii ndimo fasihi inachota maudhui na fani na kuiweka katika maandishi au katika masimulizi. Makala haya yanahusu kuchunguza dhamira ya kutenda wema katika diwani ya Mashairi ya Saadani Kandoro na hivyo nadharia ya Sosholojia ya fasihi ni muafaka katika uchambuzi wa data za makala haya kwa sababu dhamira hii ni suala la kijamii ambalo kikawaida huchunguzwa kwa kutumia nadharia za kijamii.

**3.1 Methodolojia ya Makala**

Methodolojia ni mbinu za utafiti ambazo ndizo hueleza na kubainisha namna data za utafiti zitakavyokusanywa kisayansi ili kutimiza malengo mahususi ya utafiti. Data za makala haya zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini ambapo kwa mujibu wa Babbie (1999) anaeleza kwamba, usomaji makini ni mbinu ya kukusanya data kutoka katika matini iliyoandikwa kwa mtafiti kusoma kwa makini kwa lengo la kupata data zitakazokidhi malengo ya utafiti wake. Kupitia mbinu hii mtafiti aliongozwa na hatua tano za kukusanya data kwa kutumia mbinu hii. Hatua ya kwanza ilikuwa ni kuisoma diwani husika ili kuona ni dhamira gani zinapatikana ndani yake, hatua ya pili ikawa ni kusoma na kuchnukuwa sehemu ya madondoo ambayo yanajenga dhamira, hatua ya tatu ikawa ni kuunda vichwa na mada kwa ajili ya kuweka madondoo yenye data kila moja mahali pake stahiki, hatua ya nne ikawa ni kuweka data zinazofanana pamoja na kuweka zinazotofautiana pembeni na hatua ya tano ikawa ni kuzipangilia data katika mpango rahisi wa kuzichambua.

Data za makala haya zimechambuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo ambapo data zimechambuliwa kwa kupewa maelezo yenye kuendana na lengo la makala ambalo ni kuchunguza dhamira katika diwani ya Mashairi ya Saadani. Data zimewasilishwa kupitia madondoo ya mishororo na beti za mashairi, madondoo hayo yamepewa maelezo, maelezo yamehusishwa na nadharia na mwisho hoja kuhusu data husika zimehitimishwa.

**4.1 Dhamira katika diwani ya Mashairi ya Saadani**

Katika sehemu hii tumewasilisha dhamira ya kutenda wema ambayo inapatikana katika diwani teule kulingana na lengo la makala yetu kama ifuatavyo:

**4.1.1 Dhamira ya kutenda wema**

Binadamu ni kiumbe mwenye uhusiano na wanadamu wengine katika kufanikisha masuala mbalimbali katika maisha yake ya kila siku. Hakuna binadamu ambaye anaweza kuishi mwenyewe bila kuwa na uhusiano na wanadamu wengine na uhusiano huo unaweza kuwa katika masuala ya kijamii, kisiasa, kiutamaduni na kijamii. Uhusiano huu ni muhimu sana na unaweza kufanikiwa kutokana na wahusika kutendeana wema na si vinginevyo. Dhamira ya kutenda wema katika Mashairi ya Saadan imewasilishwa kupitia shairi la "Binadamu Tenda Wema," lililopo ukurasa wa 18 ambapo inasemwa:

1. Nitungayo si mabaya, ni mafunzo ya hekima,
   Mtu asiye na haya, huyo si mtu ni kima,
   Asiyejua vibaya, ni mjinga wa heshima,
   Binadamu tenda wema, japo utendewe ubaya.

2. Someni mkipokeya, kichwani mkiyapima,
   Wajinga watachukiya, nakuyaona si mema,
   Mkosa jema tabiya, umuepuke mapema,
   Binadamu tenda wema, japo utendewe ubaya.
   …
3. Japo utendewe ubaya, binadamu tenda wema,
   Kwa vitendo na hekaya, uwe mtu wa huruma,
   Uwaombee wabaya, wapate tabia njema,

 Copyright: © 2026 by the authors. Submitted for possible open access publication under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution (CC BY) license (https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/).

Binadamu tenda wema, japo utendewe ubaya.

Katika beti hizi tatu za shairi la "Binadamu Tenda wema," tunaona dhamira ya kumtaka binadamu kutenda wema ikijitokeza kwa mawanda mapana kabisa. Maneno, "Binadamu tenda wema, japo utendewe ubaya," yanajitokeza tangu katika kichwa cha shairi na baadae katika kibwagizo cha kila ubeti. Hii inasaidia kutoa msisitizo juu ya umuhimu wa kutenda wema katika maisha ya binadamu ambapo inatajwa kuwa kutenda wema humfanya mtu kuwa na heshima katika jamii. Ubeti wa kwanza unamtaja mtu asiyependa kutenda wema kama mtu ambaye hana heshima na kumfananisha sawasawa na mnyama. Ubeti wa pili unatoa msisitizo kuwa njia ya kuepuka uovu au watu waovu ni kutenda wema. Hii inajenga picha kuwa, katika jamii wapo watu ambao daima hutenda ubaya lakini wakifanyiwa wema kwa upande wa pili wanaweza kubadilika nao wakawa ni watenda wema. Msitari huu "mkosa njema tabiya, umuepuke mapema," ndiyo inayotupatia picha kwamba kutenda wema ni silaha ya kuwaepuka wabaya kwani nao huona haya kurudisha ubaya kwa mtu aliyewatendea wema. Wanasosholojia wanasisitiza kuwa ni wema daima ndiyo huifanya jamii kuwa na furaha na amani katika maisha na ubaya na uadui ni vitu ambavyo huifanya jamii kukosa amani na kuishi maisha duni na yenye simanzi.

Ubeti wa nne wa shairi hili kupitia maelezo ya "Binadamu tenda wema, japo utendewe ubaya," inaeleza kuwa kutenda wema ni vitendo na huruma ambayo mtu huwa nayo kwa watu wengine. Vitendo vinaweza kuwa vya aina mbalimbali kama vile kuwasaidia wale wasiojiweza, kuwahurumia, kuwasomesha watoto wa masikini na wale wa mitaani. Pia, kutenda wema ni pamoja na kuwaombea dua njema watenda mabaya wabadilike na kuwa na tabia njema. Hii ni darja ya juu ya mtu mwenye kutenda wema katika jamii na kama kila mwanajamii akiwa na hulka na tabia kama hii ni dhahiri kuwa maisha yatakuwa mazuri yenye furaha na baraka tele. Katika ubeti wa saba wa shairi husika mtunzi anasema:

7. Ukitendewa ubaya, nawe ukatenda wema,
Yawe yako mazoweya, maisha dumu daima,
Kwa mola nakuapiya, utakuwa na heshima,
Binadamu tenda wema, japo utendewe ubaya.

Binadamu anatakiwa kutenda wema katika maisha yake ya kila siku hata kama akitendewa ubaya na watu wengine. Jambo hili limerudiwa mara nyingi katika shairi husika na kwa kutumia methali "Binadamu tenda wema, japo utendewe ubaya," kitu kinachoashiria kuwa wema ni kitu chenye nguvu kubwa ya kuubadili ulimwengu kuwa mahali pazuri pa kuishi na kila mtu akawa furahani. Hata hivyo, jambo la kuijiuliza ni kuwa hivi katika jamii ni rahisi kumpata mtu huyo? Yaani mtu ambaye anatenda wema tu hata kama anatendewa ubaya tena kila siku katika maisha yake. Wanasosholojia wanasema kuwa binadamu ni kiumbe ambaye anachoka haraka na kukinai mambo ikiwemo hili la kutenda wema na kutendewa ubaya. Ni binadamu wachache sana katika ulimwengu wa leo ambao wanaweza kuwa na tabia ya uvumilivu wa aina hii na kiuhalisia hawapo kabisa watu hao katika ulimwengu wa leo. Hata hivyo, ni muhimu kuendelea kuhamasisha watu kutenda wema kwani katika wengi wapo wachache ambao wanaweza kubadilika na kuwa na mwenendo mzuri wa kutenda wema na kuachana na mabaya.

Dhamira ya wema inajitokeza pia katika methali namba katika shairi la "Utu ni koja na taji," ukurasa wa 79 ambapo mshairi anasema:

1. Utu ni koja na taji, koja ni kwa mtu mke,
Mtu mke huhitaji, taji pia tumvike,
Na mume anataraji, taji kwako tuliweke,
Uaminifu tushike, utu ni koja na taji
…
4. Nawe muombe mpaji, kwa watu uaminike,

 Copyright: © 2026 by the authors. Submitted for possible open access publication under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution (CC BY) license (https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/).

Tupewe wote vipaji, ya ovyo tusiropoke,
Tuombe kwa muombaji, mema yasituponyoke,
Uaminifu tushike, utu ni koja na taji.

Beti hizi mbili zinaendelea kutoa msisitizo juu ya umuhimu wa wanajamii kutenda wema kupitia matendo yao na si maneno pekee. Mshororo "Utu ni koja na taji," inaeleza kuwa utu wema huenda sambamba na matendo mema ambapo binadamu hupata heshima kutokana na vitendo au matendo yake ya kiutu. Haiwezekani mtu akawa anazungumza maneno mazuri lakini anatenda maovu akawa ni mtu mwema katika jamii. Mtu wa aina hii hupuuzwa na kuonekana kuwa hana maana na watu humdharau. Katika maisha halisi ya jamii mbalimbali duniani wapo watu ambao kazi yao kubwa ni kusema zaidi na hasa katika kuhamasisha watu kutenda mema lakini wao binafsi wanakuwa ni watenda maovu. Wanasosholojia wanaeleza kuwa, si jambo jepesi kwa binadamu kuendana au kutekeleza kile anachosema kwa asilimia 100 isipokuwa kwa watu wachache sana. Hii ni kwa sababu binadamu ni kiumbe ambaye anapenda kuona mambo yanakuwa vizuri lakini kuna suala la matamanio ya nafsi yake ambayo mara nyingi humfanya binadamu kutamani kufanya mambo ambayo kimsingi hayakubaliki katika jamii yake. Nafsi hiyo ya matamanio inapomzonga na kumshinda nguvu ndio hapo sasa hata ile hali ya kutenda kama alivyokuwa akisema inakuwa haipo tena. Hata hivyo, ingawa uhalisia upo hivyo kwa kiasi kikubwa wapo baadhi ya watu wachache ambao wanajitahidi kutenda mema kwa kadri ya uwezo wao na jamii inatambua hivyo.

**4.2 Hitimisho**

Dhamira ya binadamu kutenda wema imejitokeza kwa kiasi kikubwa katika diwani ya Mashairi ya Saadan ambapo tumeona mashairi mawili yakielezea dhamira hii. Itakumbukwa kwamba, diwani hii iliandikwa katika kipindi cha ujamaa na kujitegemea wakati wa Azimio la Arusha ambapo jamii ilitakiwa kuwa kitu kimoja kwa kuishi kwa upendo wa hali ya juu. Kutokana na jamii kutoka katika kipindi cha ukoloni ambapo watu waliishi maisha ya shida yaliyojaa dhuluma iliyofanywa na wakaloni ilikuwa ni busara na hekima kuwataka wananchi kuishi pamoja ili kujenga upendo kwa kutendeana wema baina yao. Hii haikuwa kwa Tanzania peke yake bali kwa mataifa mengi ya Bara la Afrika na kwingine ulimwenguni kote walikotawaliwa na wakoloni. Mshairi Saadan Kandoro ametimiza wajibu wake wa kuihamasisha jamii iishi kwa kutendeana wema baina yao.

**MAREJELEO**


[1] Abeid, A. (1954) *Sheria za kutunga mashairi na Diwani ya Amri.* Nairobi: East Africa Literature Bureau.

[2] Babbie, E. (1999) *The basics of social research*. Belmont: Wadsworth Publishing Company.

[3] Babusa, H. O. (2005) "*Vigezo badilia kuhusu uainishaji wa mashairi ya Kiswahili*". Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

[4] Kandoro, S. A. (1972) *Mashari ya Saadan*. Dar es Salaam: NPL.

[5] Kezilahabi, E. (1974) *Kichomi*. Nairobi: Heinnemen.

[6] Kezilahabi, E. (1977) "Mashairi ya Saadan", katika *Mulika, Namba 14*. Dr es Salaam: TUKI. Kur. 32-40.

[7] Kitogo, S. A. (2002) "The poets contribution to political development: A case of Saadan Abdul Kandoro," Unpublished *M.A. Thesis* UDSM.

[8] Masinde, E. (2003) "Ushairi wa Kiswahili, maendeleo na mabadiliko ya maudhui," Tasinifu ya uzamivu ya Chuo Kikuu Cha Kenyatta.

[9] Mulokozi, M. M. (1975) "Revolution and reaction in Swahili poetry". *In Kiswahili, Vol. 45/2.* Dar es Salaam: IKR, Kur. 46-65.


 Copyright: © 2026 by the authors. Submitted for possible open access publication under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution (CC BY) license (https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/).

[10] Mulokozi, M. M. na Sengo, T. S. Y. (1995). *History of Kiswahili Poetry* [AD 1000-2000]. Dar es Salaam: TUKI.
[11] Mulokozi, M. M. & Kahigi, K. K. (1976) *Malenga wa Bara*, Dar es Salaam: EALB.
[12] Njogu na Chimerah, C. (1999) *Ufudishaji wa fasihi, nadharia na mbinu.* Nairobi: JKF.
[13] Omary, M. (2011) "Siasa katika ushairi wa Kezilahabi: Uchunguzi wa *Karibu Ndani* (1988) na *Dhifa* (2008)", Tasinifu ya uzamili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
[14] Omary, M. (2015) "Kuchunguza ufasihi simulizi katika kazi za Euphrase Kezilahabi: Mfano wa vitabu vya *Kichomi*, *Karibu Ndani* na *Dhifa*," Tasinifu ya Uzamivu ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.
[15] Senkoro, F. E. M. (1988) *Ushairi, nadharia na tahakiki*. Dar es Salaam University Press.
[16] Wamitila K. W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi*: *Misingi na Vipengele Vyake*, Nairobi: Poenix Publisher Ltd.
[17] Wamitila K. W. (2008) *Kanzi ya fasihi*: Misingi ya uchanganuzi wa fasihi. Nairobi: Vide – Muwa.

Disclaimer/Publisher's Note: The statements, opinions, and data contained in all publications are solely those of the individual author(s) and contributor(s) and not of **AJHAS** and/or the editor(s). **AJHAS** and/or the editor(s) disclaim responsibility for any injury to people or property resulting from any ideas, methods, instructions, or products referred to in the content.

 **Copyright: © 2026 by the authors. Submitted for possible open access publication under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution (CC BY) license (https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/).**